



BODI YA MKONGE TANZANIA

TANGAZO LA KUKARIBISHA MAOMBI YA MASHAMBA YA KULIMA MKONGE

1.0 Utangulizi

Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) inawatangazia watanzania wote kuwa inatarajia kugawa mashamba kwa ajili ya kilimo cha mkonge kwa wakulima wadogo ili kuendeleza kilimo cha mkonge nchini. Mashamba yanayokusudiwa kugawiwa kwa wakulima wadogo ni mashamba ya Hale Estate, Magoma Estate, Magunga Estate, Ngombezi Estate na Mwelya Estate yaliyopo Wilaya za Handeni na Korogwe ambayo yanamilikiwa na Bodi ya Mkonge Tanzania ambayo sehemu yалишагавиwa kwa wakulima wadogo.

2. Utaratibu wa Maombi ya mashamba

Waombaji wote watatakiwa kujaza fomu maalum inayopatikana katika ofisi za Bodi ya mkonge na katika tovuti ya www.atmis.kilimo.go.tz. Baada ya kujaza, fomu irejeshwe katika ofisi za Bodi ya Mkonge Tanzania zilizopo Kiwanja Na.65 jengo la Mkonge (Mkonge House), Barabara ya Uhuru/Usagara,Tanga Jiji, kabla au ifikapo **tarehe 01 Januari 2020** au tuma kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi mkuu,
Bodi ya Mkonge Tanzania,
S.L.P 277 Tanga.
Barua pepe: dg@sisalboard.go.tz

3. Masharti ya uombaji

Masharti ya uombaji wa mashamba ni kama yalivyoainishwa kwenye fomu ya maombi. Waombaji wote waliowasilisha maombi Bodi ya Mkonge kwa njia ya barua wanaelekezwa kuwasilisha upya maombi yao kwa utaratibu wa kujaza fomu. Inasisitizwa kuwa maombi yote ya shamba yatakayowasilishwa au yaliyokwishawasilishwa nje ya utaratibu wa ujazaji wa fomu hayatashughulikiwa. Maombi yatashughulikiwa kwa utaratibu wa "**Wa kwanza kuomba wa kwanza kushughulikiwa**" (*first in first served*) *kutegemea na upatikanaji wa eneo*.

Limetolewa Na:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Mkonge Tanzania,
S.L.P 277,
TANGA.